# MARK
# MTAALA

## I. MAELEZO KWA UJUMLA.

A. Mwalimu: Chuck Homer

B. Mtafsiri Chris Mwakabanje.

C. Kozi hii ni jumla ya masomo 12 katika SP 4 za kaseti za video (au PA 2 za kaseti za video).

D. Kila somo linachukua takribani dakika 38.

## II. MAELEZO NA MALENGO.

A. Kozi hii imekusudiwa kujifunza kitabu cha Marko ili kubainisha namna ya kuongeza imani katika Yesu kama Mwana wa Mungu.

B. Mwanafunzi atakuwa tayari kuwafundisha watu wengine kitabu hiki.

## III. VIFAA MUHIMU.

A. Unapaswa uwe na:

1. Biblia (UV, ASV, KJV, AU NKJV).
2. Masomo 12 ya video.
3. Notisi za kozi hii.

B. Maoni.
Fafanuzi (commentary) yoyote ile katika kitabu cha Marko.

## IV. MAMBO YA KUFANYA KATIKA KOZI HII.

A. Soma kitabu chote cha Marko angalau mara moja.

B. Tazama (view) masomo yote 12 kwa njia ya video.

C. Soma notisi zote za darasa.

D. Dondoa mistari yote (maelezo hapo chini).

E. Wakilisha makala ya muhula (malezo hapo chini).

F. Fanya mtihani mmoja uliochapwa.

G. Uwe na wastani wa maksi 70 angalau.

## V. KAZI YA KUDONDOA.

A. Dondoa lazima ziandikwe (ama kuchapwa) bila kutazamia, kisha kuzituma kwa VBI kwa ajili ya kusahihisha. Mistari sharti itoke katika UV kama ulivyoonyeshwa katika fomu yako ya maombi ya kujiunga na VBI.

B. Mistari sharti iandikwe ama ichapwe wakati mmoja (mkao mmoja). Unaweza kujifunza zaidi na kuirudia upya yote kama ulikosea, lakini unatakiwa uanze upya yote katika mkao mmoja.

C. Kwa kozi hii mistari hii ni lazima idondolewe:

| | | |
|---|---|---|
| 2:17 | 8:34-36 | 11:25,26 |
| 7:6,7 | 9:1 | 12:29-31 |
| 7:37 | 9:23 | 16:15,16 |

D. Kazi ya kudondoa itatakiwa wakati unapotuma mtihani wako uliochapwa kwa VBI.

E. Maoni: Njia bora ya kudondoa ni kuandika mistari katika vijikadi ili kwamba iwe rahisi kwako kuirudia-rudia muda wote unavyoendelea na kozi hii.

## VI. MITIHANI.

A. Kuna mtihani mmoja wa kuchapwa mwishoni mwa kozi ya Marko.

B. Utakapokaribia mwishoni tafadhari wasiliana nasi na uombe mtihani tukutumie.

C. Utakapopata mtihani unaruhusiwa kuupitia na kujifunza.

D. Walakini, unapofanya mtihani lazima uufanye bila kutazamia kabisa kutoka katika notisi, Biblia, kitabu, n.k.

## VII. MAKALA YA MUHULA.

A. Andika makala ukibainisha Uungu wa Yesu kutoka katika kitabu cha Marko. Toa hoja kutoka katika mafungu mbalimbali katika Marko ukibainisha kuwa hakika Yesu ni Mwana wa Mungu.

B. Makala ni sharti iwe na wastani wa kurasa nne, zilizochapwa kuacha nafasi mbili mbili (double spaced). Kama umeandika kwa mkono makala isizidi kurasa sita, bila kuacha nafasi ya mstari (single spaced).

C. Makala yatahitajika wakati unatuma mtihani wako wa mwisho na kazi ya dondoa VBI.

**VIII. MAKSI.**

A. Kazi ya kudondoa, makala ya muhula na mtihani vitasahihishwa tofauti-tofauti.

B. Matokeo ya mwisho yatategemea wastani wa kazi zote ulizopewa, mtihani ukihesabiwa mara mbili.

C. Unaweza kuomba ili ufafanuliwe kuhusu maksi au ufikiriwe, lakini kwa vyovyote vile VBI ndiyo yenye kutoa uamuzi wa mwisho.

**IX. TUNZO.**

A. Tunzo itatolewa, ikiwa ni pamoja na cheti, pale tu utakapomaliza kikamilifu kazi zote, kurudisha kaseti zote (kama uliazima) na kulipa ada zote kwa kozi hii.

B. Mungu na akubariki unapojifunza maneno yake yenye uvuvio!

## MARKO
## MAZINGIRA

**I. UANDISHI: YOHANA MARKO.**

A. Mwandishi wa kitabu hajitambulishi mwenyewe.

B. Kanisa la awali lilimtaja mwandishi kuwa ni Yohana Marko.

C. Mapokeo yanataja kuwa Marko alikuwa na Petro Rumi (?).

1. Alikuwa mshiriki mwaminifu aliyesafiri pamoja na Petro (1 Petro 5:13).
2. Justin Martyr anainukuu injili hiii na kuiita "Mahubiri ya Petro" (Memoirs of Peter).
3. Wengine, karibu na karne ya kwanza, wanadai Marko aliyapata mambo mengi aliyoandika moja kwa moja toka kwa Petro.

II. **INSHA: YESU NI MTUMISHI WA MUNGU MWENYE MATESO** (linga. 8:31; 10:33).

A. Marko anatoa moja ya sababu za kifo cha Yesu:

1. Ukombozi kwa ajili ya wengi – 10:45.
2. Kwa ajili ya msamaha wa dhambi – Mt.26:28.
3. Kwa ajili ya kondoo – Yohana 10:11.

B. Isaya 52:13-53:12 ni mazingira yanayolingana na injili hii ya Marko.

**III. 55-70 B.K.**

A. Ni vigumu kutambua tarehe haswa.

B. Papius, akielezea mapokeo, anasema kanisa lililokuwa Rumi lilimtaka Marko aandike injili hii kama mahubiri aliyofundisha Petro.

**IV. KUSUDI: INJILI KWA MATAIFA, HASA WARUMI.**

A. Inaondoa mambo mengi haswa walipenda Wayahudi na kufafanua utamaduni na lugha ya Kiyahudi kwa wasomaji wasio Wayahudi (5:41; 7:34; 15:34).

B. Kitabu hakitoa msisitizo katika unabii wa Agano la Kale kama ilivyo kwa Mathayo na Yohana.

C. Picha ya Yesu Marko anayoiwakilisha inadhihirika katika akili za Warumi.

1. Mwana wa Adam ameonyeshwa katika mtu mwenye kuchukua hatua zenye nguvu.
   a. Yesu anaonyeshwa kama mfanya kazi hodari akifanya mambo kwa haraka kutoka kazi moja hata nyingine.
   b. Neno la Kiyunani **ευφεωσ** lililotafsiriwa kama “mara, ghafula au mara moja." Kati ya hizo, mara 14 limetumika likitaja kazi za Yesu mwenyewe.

2. Kazi zake za ujasiri kwa wengine na kupenda kwake kufa kwa ajili ya wengine kungewavutia Warumi kusikiliza.

3. MATENDO ni ufunguo kwa injili hii. Kutokana na wazo hilo akilini watu wengi hudhania injili hii iliandikwa awali kwa Warumi waliokuwa wachapa kazi na wenye kujivunia mafanikio yao.

**V. MUUNDO: INJILI.**

**VI. SISITIZO NA SIFA MAALUMU.**

A. Mambo kadhaa yaliondolewa na Marko kama ambayo hayakuhitajika katika ujumbe wake maalum.

1. Hakuna ukoo wa Yesu,
2. Hakuna kuzaa kwake bikira, na
3. Hakuna habari za Yesu za utoto wake.

B. Marko anakazia mambo yaliyotendeka zaidi kuliko hoja na masomo.

C. Nukuu za Agano la Kale.

1. Mara moja tu Marko ananukuu moja kwa moja toka katika Agano la Kale – 1:2,3.
2. Na anamnukuu Yesu tu akinukuu hayo mara mbili.

D. Anatoa mifano 8 pekee kati ya inayowezekana 70.

E. Anataja mara 23 watu mbalimbali walivyomjibu Yesu.

F. Ukaribu wa Marko na Petro.

1. Kielelezo na mazingira ya hotuba ya Petro katika Matendo 10:34-43 inalingana sana na injili hili.

2. Injili hii, ukiondoa Yohana Mbatizaji, inaanza na kuitwa kwa Petro.

3. Jina la Petro linajitokeza katika 1:36, 11:21; 13:3 na wala si katika vitabu vingine vya injili zenye habari kama hizi.

4. Petro anapotoka gerezani anakwenda nyumbani kwa mama yake Marko.

5. Mambo haya yote iwapo yanalenga uhusiano wa karibu na Petro, ni kawaida kudai kwamba Marko alitumia muda mwingi wakiwa pamoja.

6. Ni dhahiri, hakika, kwamba Yohana Marko aliyapata mambo mengi kutoka kwa Petro.

7. LAKINI, usisahau – bado Roho Mtakatifu ndiye aliyeongoza kuandikwa kwa injili hii!

G. Marko anatumia nyakati za kihistoria zilizopo 151 zinazotilia mkazo vitendo.

H. Ingawa injili hii ndiyo fupi, inabainisha zaidi maeneo fulani fulani kuliko injili zingine. (1:14-29; 6:14-19; 7:1-23; 12:28-34).

I. Kwa kadiri tujuavyo injilli hii kwa ujumla imeandikwa kwa mpangilio wa nyakati (chronological).

J. Kijana asiyetajwa jina aliyekimbia kutoka bustanini katika 14:51,52. Ukweli huu umetolewa kama fafanuzi ya tukio, lakini wengi hudhania Marko anaelezea tendo lake mwenyewe wakati huo.

## VII. HUDUMA YA YOHANA MBATIZAJI.

A. Yohana anagusia kwa uzito zaidi kazi ya Yohana Mbatizaji na hata kutaja muda wa "mwanzo wa injili ya Kristo" kutoka kwake (1:1).

1. Wote wawili Petro na Paulo wanataja bayana huduma ya Yohana Mbatizaji kama mwanzo wa injili (Mdo.10:36,37; 13:23,24).

2. Yesu pia alitambua umuhimu wa Yohana Mbatizaji (Lk.16:16).

B. Agano la Kale linahatimisha na unabii wa kuja kwake Yohana (Mal.3:1; 4:5,6).

C. Kazi ya Yohana ilikuwa kuwaandaa watu kwa ajili ya kazi ya Masihi (1:1,2).

D. Ujumbe wa Yohana Mbatizaji ulikuwa watu watubu na kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi (1:4 linga. Mt.3:2).

## VIII. KAZI YA MITUME.

A. Majina ya mitume yametajwa mara nne katika Agano Jipya:
1. Mt. 10:2-4.
2. Mk. 3:16-19.
3. Lk. 6:14-16.
4. Mdo. 1:13.

B. Walifanya kazi muhimu sana kwa ajili ya Bwana – linga. Mt. 18:18; Efe.2:20; Ufu.21:14.

C. Neno mitume limetumika kwa njia mbili katika Agano Jipya.

1. Kwa namna ambayo si ya kiufundi linarejea mtu yeyote ambaye anafanya kazi chini ya mamlaka – Matendo 14:4, 14; 1 Thes.1:1 linga.2:6.
2. Linapolenga yeyote kati ya kumi na mbili au Paulo, linamaanisha haswa mwenye mamlaka ya kutenda kama wakili kwa niaba ya Yesu Kristo – 2 Kor.5:20.

D. Kusudi la Yesu katika kuwachagua mitume limebainishwa katika 3:14,15.
1. Walipaswa kuwa pamoja naye, wajifunze kutoka kwake na kushuhudia matukio ya huduma yake, kifo na ufufuo – Mdo. 1:21,22.
2. Walitakiwa kuwa wajumbe wa ufalme wa Mungu.

3. Walipaswa kutiwa nguvu toka kwa Roho Mtakatifu ili kutenda miujiza kama swala la kuitambulisha kazi yao.

E. Kazi yao haikuwa ya kudumu katika kanisa.
   1. Mathiya alichaguliwa ili kuijaza ofisi iliyoachwa wazi na aliyekengeuka iliyotokea kabla ya kifo cha Yesu.
   2. Ofisi zingine za mitume hakubadili yeyote mara baada ya kifo cha mtume mwenyewe.

## IX. TATIZO LA FUNGU LA 16:9-20.

A. Mistari hii haipatikani katika baadhi ya maandishi ya kale ya Kiyunani (manuscripts) ambayo hupatikana leo.

B. Hii ndiyo sababu baadhi ya tafsiri huondoa, na kuchapa pembezoni mwa kurasa (margin) ama pengine kuonyesha kuwa hili ni tatizo la fungu.

C. Mistari hii ama kuwa hapa au kutokuwepo haituathiri sisi au imani yetu kwa njia yeyote ile. Hakuna katika imani au mambo ya kufanya katika Ukristo ambayo husimamia au kuangukia katika mistari hii 12. Kila kitu kinachopatikana katika mistari hii kinapatikana pia katika mistari mingine ya Agano Jipya.

## X. HISTORIA YA KIPINDI CHA KATI YA MAANGANO.

A. Wagalatia 4:4 – Ulimwengu ulioandaliwa kwa ajili ya Kristo kuja.

   1. Katika kipindi cha Malaki Yuda ilikuwa jimbo chini ya Uajemi (Persian).
      a. Muda mfupi baada ya huu Uyunani ikatawala.

      b. Homeri na Daudi waliishi katika miaka ya 1,000 K.K.

      c. Historia haswa ya Uyunani ilianza mwaka 776 K.K.

      d. Nchi yenye utamaduni wa Kiyunani 776 – 500 K.k.

      e. Plato, Socrates na Aristotle waliishi kipindi cha matengenezo ya Wayahudi (restoration period).

      f. 331 – 330 K.K. Alexander Mkuu alianza kutawala.

      g. Alexander alivamia na kutawala Palestina.

      h. Alexander alikufa mwaka 323 K.K. akiwa na miaka 33.

i. Waseleusidi (Seleucids) wakatawala Mashariki na Watolemi (Ptolemies) wakatawala Magharibi.

j. Watolemi wakatoa uhuru kwa Wapalestina.

k. Katika mwaka 198 K.K. Mseleusidi aliyeitwa Antiochus III aliitwaa tena Palestina.

l. Antiochus Epiphanies IV alitawala 175 – 164 K.K.

m. Katika mwaka 168 Antiochus Epiphanies IV:
   1) Alitoa ngurume madhabahuni katika hekalu.
   2) Akapaka damu katika kuta za hekalu.
   3) Akafanya na sanamu ya sayari ya Jupiter na kuiweka hekaluni.
   4) Alikataza ibada za hekaluni.
   5) Alizuia tohara.
   6) Aliangamiza kila nakala ya maandishi ya Kiyahudi aliyoweza kuiona.
   7) Aliuza familia nyingi za Kiyahudi utumwani.

n. Kipindi cha Makabayo (Hosmonean) kilitokea mwaka 165 – 63 K.K.

   1) Kuhani, Mattathias, na watoto wake 5 walikasirika na kurejesha utawala wa Palestina.
      a) Yuda alitawala 166 – 161 K.K.
      b) Johnathan alitawala 161 – 144 K.K.
      c) Simon alitawala 144 – 135 K.K.
      d) Yohana.
      e) Eliazer.

   2) Katika mwaka 165 K.K. Yuda na familia yake waliutwaa Yerusalem na kulisafisha hekalu. Hili likazidua sikukuu ya Kutabaruku (Yoh.10:22).

   3) Yohana Hyrcanus (mwana wa Yohnathan) alitawala 135 -106 K.K. (pamoja na utawala wa watoto wake).

   4) Aristobulus I alitwaa cheo cha mfalme. Utawala wake ni pamoja na watoto wake, ilikuwa 106 – 63 K.K.

   5) Jina Makabayo linamaanisha “nyundo.”

6) Wayahudi walikuwa huru katika miaka 165 – 63 K.K.

o. Katika 63 K.K. Pompeii alitwaa Palestina.

1) Antipater, baba yake Herode Mkuu, aliteuliwa kutawala katika Palestina na akatawala hadi 43 K.K.

2) Walikuwa Waidumia (Idumean)

p. Herode Mkuu alifanyika kuwa mtawala wa palestina 37 K.K. Alianza kujenga upya hekalu ili kupata kibali kutoka kwa Wayahudi.

B. Mabadiliko ya lugha.

1. Kipindi cha karne ya kwanza lugha ya Wayahudi ilikuwa ni Kiarami (Mk.5:41; 7:34).

2. Kulikuwa na watu wengi ambao hawakuweza kusoma Kiebrania.

3. "Targums" ni tafsiri ya Kiarami ya maandishi ya Kiebrania (takribani 200 K.K.).

4. "Targums" iliandikwa karne ya pili ikiwa pamoja na maoni yaliyoongezwa.

5. Talmud (simulizi za mapokeo) yalianza na kuandikwa muda huo huo.

C. Masinagogi yalianza kipindi hiki.

1. "Sinagogi kuu" lilikuwa jina lililotolewa kwa watu 120.
   a. Nehemia alilianzisha sinagogi hili pamoja na Ezra kama mkuu mwaka 410 K.K.
   b. Kusudi lake ilikuwa kuwaongoza waliotoka uhamishoni kuingia katika Uyahudi wa kweli.
   c. Lilifikia mwisho mwaka 275 K.K.

2. Masinagogi pia yaliibuka kutokana na hitaji la Wayahudi waliotawanyika ili kuongozwa hata kuufika Uyahudi wa kweli.

3. Baraza (Sanhedrin – bodi ya uongozi katika Wayahudi).

   a. Linadhania kuanza katika karne ya tatu K.K. 2 Nya.19:5-11 inaonyesha kuwa lilianza mapema zaidi.

   b. Chini ya Warumi uwezo wa kutoa hukumu ya kifo baraza lilinyang’anywa.

D. Mielekeo aina tatu ya dini ya Kiyahudi karne ya kwanza.
   1. Yenye kufuata sheria haswa (legalistic).
   2. Mapokeo (mapokeo kuwa sawa na neno la Mungu) na
   3. Kitaifa (nationalistic).

E. Utamaduni wa wakati huo.
   1. Nyumbani.
      a. Chimbuko la kila kitu.
      b. Kuheshimika wakati wa uzee.
      c. Daima walishukuru kwa ajili ya chakula.
      d. Kula chakula lilikuwa jambo la kawaida familia kujumuika pamoja.
      e. Kuzaliwa lilikuwa swala la baraka kwa familia, haswa ikiwa ni mtoto wa kiume.
         1) Angeendeleza jina la familia.
         2) Kuwa mtu wa kutafuta mkate.
         3) Kuilinda familia.
         4) Nguvu kwa taifa.
         5) Ikiwa familia ilikuwa ya kabila ya Yuda, lilikuwepo tumaini kwamba pengine ni Masihi.

   2. Ndoa.
      a. Mipango ya ndoa ilifanywa na familia ama marafiki.

      b. Kuposa ilikuwa jambo la sheria (binding).

      c. Sherehe za ndoa zilikuwa si zaidi ya kumleta bibi harusi kutoka nyumbani kwa baba yake hadi nyumbani kwa bwana harusi. Yer. 7:34; 16:9; Mt.22:11; Yoeli 2:16; Mwa.29:23.

      d. Kumkomboa mtoto wa kiume kulifanywa katika siku 40 na wa kike katika siku 80.

      e. Mara baada ya mtoto kukua alipitia hatua mbalimbali.

1) Katika umri wa miaka 5 alianza kujifunza kusoma Biblia ya Kiebrania (Shema – Kumb.6:4).
2) Kisha akaanza kujifunza vitabu vitano vya Musa (Pentateuch).
3) Akiwa na umri wa miaka 10 aliongeza Mishna.
4) Akiwa na miaka 13 alipitia Bar Mitzvah ("Mwana wa amri).
5) Katika umri wa 15 alianza kujifunza Talmud.
6) Umri wa miaka 18 kwa kawaida alioa \ olewa.
7) Miaka 20 alifanya kazi katika kazi yake ya maisha.

f. Wasichana walijifunza mambo ya ufundi ya nyumbani.

F. Makundi mbalimbali ya jamii. Kutoka juu hadi chini.

1. Masadukayo (daima waliongoza baraza la Sanhedrin).

2. Farisayo.

3. Watoza ushuru.

4. Wenye dhambi.

5. Myahudi wa chini kabisa alikuwa mtumwa.

6. Askari wa Rumi na watumishi.

7. Wafanya biashara wa Mataifa.

8. Wasamaria.

G. Kifo.

1. Waombolezaji wazoefu walialikwa na watu matajiri.
2. Mwili ulioshwa na kupakwa mafuta, n.k., kisha kuzungushiwa na sada.

H. Madhehebu.

1. Mafarisayo – kundi la hiari la viongozi.
   a. Ndilo lilikuwa likiongoza zaidi kipindi cha Yesu – karibu 6,000.
   b. Walikuwa jamii iliyoungana kwa karibu sana, n.k.
   c. Walipenda siasa kwa kiasi kidogo kabisa.
   d. Walisisitiza mambo madogo na utu wa nje wa mtu

2. Masadukayo – wenye mtazamo wa kisiasa.
   a. Waliamini kuwa Mungu hakujishughulisha sana na mambo ya mwanadamu.
   b. Walikuwa takribani 4,000 wakati huo.
   c. Hawakutazamia kuja kwake Masihi.
   d. Walikuwa makatili na kuchukua kila fursa walioweza kuipata katika kila hali.

3. Maherode – kwa ujumla kama chama cha siasa.
   a. Mk. 3:6 inaonyesha mfano mchache wa mahusiano kati yao na Mafarisayo.
   b. Ushirikiano huo ulikuwa na kusudi la kumwua Yesu.
   c. Hii ni mara ya kwanza waliyoweza kuungana pamoja.

4. Wazelote – kinyume kidogo na Maherodia katika mtazamo wao.
   a. Walitaka uhuru wa kisiasa.
   b. Walitumia mfumo wa uvamizi (guerrilla) katika kupambana.
   c. Kimsingi ndio waliosababisha kuharakisha maangamizi ya hekalu.
   d. Simoni mtume alikuwa mmoja wa Wazelote (Mt.10:4).

5. Wasene – hawajatajwa katika Agano Jipya.
   a. Hawakutoa dhabihu za wanyama.
   b. Hawakuweka akiba yoyote ya mali.
   c. Hawakufanya aina yoyote ya vyombo vya vita.
   d. Hawakumiliki watumwa.
   e. Walijizuia kutoa viapo.
   f. Walibadilishana mawazo.
   g. Waliwaheshimu wakubwa wao kama wazazi.
   h. Walivaa nguo nyeupe (wanaume).
   i. Walioga maji baridi.
   j. Waliimba nyimbo za sifa kabla na baada ya chakula.
   k. Waliiamini kwamba roho haifi.

l. Walitilia mkazo katika:
    1) Upendo wa Mungu.
    2) Utu wema, na
    3) Upendo wa ndugu.

m. Hawakuamini katika ndoa, kwa hiyo

n. Wakatoweka wasiwepo.

I. Viongozi.

1. Warumi.
    a. Octavius Augostus …………………………. 30 K.K. – 14 A.D.

    b. Tiberius Nero Kaisari ……………………… 14 – 37

    c. Gaius Kaligula ……………………………. 37 – 41 (aliuawa).

    d. Claudius Kaisari …….. 41-54 (aliwafukuza Wayahudi watoke Rumi).

    e. Nero Kaisari …………………………….. 54-68

    f. Gulbu …………………………. 68 (miezi 7).

    g. Otho …………………………. 69 (miezi 3).

    h. Vitellius ……………………. 69 (miezi 8).

    i. Vespasian …………………… 69-79.

    j. Titus …………………………. 79-81.

    k. Domitian …………………….. 81 – 96.

2. Viongozi katika maeneo mbalimbali.
    a. Herode Mkuu ………………………. 37 – 4 K.K.
    b. Herode Archelaus … 4 K.K. – 6 B.K. (Uyahudi – Samaria).
    c. Herode Antipas …………. 4 – 39 B.K. (Galilaya – Perea).
    d. Herode Filipo Decapolis …….. 4 K.K. – 34 B.K. (Basham).
    e. Lysanais (si Herode) ………. (Abilene)
    f. Herode Agripa I …………….. 41 – 44 (lote)
    g. Herode Agripa II …………….. (lote).

3. Maliwali wa Rumi katika Palestina
   a. Pilato …………… 14-37
   b. Feliki …………… 53-60
   c. Festo ……………. 60-62

4. Kuhani wakuu.
   a. Anasi …………………….. 6-15.
   b. Kayafa …………………… 18-36

J. Vitabu vinavyopendekezwa.

1. “From Sinai to Calvary” – Eckstein).

2. “Between the Testaments” – C. Pfeiffer.

3. “Living Word Commentary, Vol. 1 – Malherbe.

**XI. KIELELEZO.**

I. Matayarisho ya Mtumishi …………………………………….. 1:1-13

II. Huduma ya Mtumishi Galilaya …………………………….. 1:14-9:50

III. Huduma ya Mtumishi Yerusalem ………………………… 10:1-13:37

IV. Kifo, maziko, na ufufuo wa Mtumishi ……………………. 14:1-16:20

XII. KIELELEZO KWA MAPANA.

A. Matayarisho ya Mtumishi ……………………………………1:1-13

1. Huduma ya Yohana Mbatizaji ……………………… 1:1-8

2. Ubatizo wa Yesu ………………………. 1:9-11.

3. Majaribu ya Yesu ……………………… 1:12,13

B. Huduma ya Mtumishi Galilaya ………………………. 1:14-9:50

1. Mwanzo wake …………………………….. 1:14,15.

2. Kuitwa kwa wavuvi wanne ……………. 1:16-20

3. Kuponywa kwa mtu mwenye pepo mchafu ……… 1:21-28

4. Kuponywa kwa mama mkwe wa Petro na wengine wengi ...... 1:29-34

5. “Watu wote wanakutafuta” ……………… 1:35-39

6. Mwenye ukoma atakaswa ………………… 1:40 – 45

7. Kuponywa kwa mwenye kupooza ………………. 2:1-12

8. Kuitwa kwa Lawi ………………………………… 2:13-17

9. Swali juu ya kufunga ……………………………… 2:18-22

10. Bwana wa Sabato ………………………………….. 2:23-28

11. Mkono ulionyauka …………………………………. 3:1-6

12. Kufundisha na kuponya makutano ……………… 3:7-12

13. Kuchaguliwa kwa kumi na wawili ……………… 3:13-19

14. Kumkufuru Roho Mtakatifu …………………… 3:20-30

15. Mama na ndugu zake Yesu …………………….. 3:31-35

16. Mfano wa mpanzi ……………………………… 4:1-9

17. Kusudi la mifano …………………………………… 4:10-12

18. Fafanuzi za mfano wa mpanzi ……………………… 4:13-20

19. Misemo mbalimbali ya Yesu ………………………. 4:21 -25

20. Mfano wa mbegu zikikua kwa siri …………………. 4:26-29

21. Mfano wa mbegu ya haradali ……………………… 4:30-34

22. Kristo kutumia kwake mifano ……………………… 4:33,34

23. Kutulizwa kwa dhoruba …………………………… 4:35-41

24. Msaada ni kinyume na moyo ulionyamaa ………. 5:1-20

25. Miujiza miwili: Yesu kumponya binti ya Yairo, na mwanamke aliyegusa vazi la Yesu …………….. 5:21-43

26. Kukataliwa kwa Yesu Nazareti ………………. 6:1-6

27. Agizo kwa wale kumi na wawili ……………. 6:7-13

28. Sherehe ya Herode na kifo cha Yohana …….. 6:14-29

29. Kulishwa kwa watu elfu tano ……………… 6:30-44

30. Kutembea juu ya maji ……………………. 6:45-52

31. Uponyaji Gennesaret …………………….. 6:53-56

32. Mambo ya ibada ni kinyume na unajisi halisi …. 7:1-23

33. Imani ya mwanamke Msirofoinike yazawadiwa …… 7:24-30

34. Kiziwi aponywa ……………………….. 7:31-37

35. Kulishwa kwa watu elfu nne ……….. 8:1-10

36. Kutamani kwao ishara kwa kemewa ……… 8:11-13

37. Chachu ya Mafarisayo na Herode …………. 8:14-21

38. Kuponywa kwa kipofu ……………………… 8:22-26

39. Kukiri kwa Petro na agizo kali la Yesu …… 8:27-30

40. Kutari mara ya kwanza wa kifo na ufufuo wa Yesu ……. 8:31-9:1

41. Kugeuka sura kwa Yesu ……………………….. 9:2-13

42. Kuponywa kwa kijana mwenye kifafa ………. 9:14-29

43. Kutabiri mara ya pili wa kifo na kufufuka wake Yesu ….. 9:30-32

44. Ni nani aliye mkuu? ………………… 9:33-37

45. Asiye kinyume nasi yu pamoja nasi …… 9:38-41

46. Msiingie majaribuni ………………. 9:42 – 50

C. Huduma ya Mtumishi Yerusalem ………………………. 10:1-13:37

1. Mafundisho juu ya talaka ………………………. 10:1-12

2. Yesu na watoto ……………………………. 10:13-16

3. Hatari ya utajiri na thawabu ya dhabihu ………. 10:17-31

4. Kutabiri kwa tatu kwa kifo na kufufuka kwake Yesu …. 10:32-34

5. Ombi la wana wa Zebedayo ………………. 10:35-45

6. Kuponywa kwa Bartimayo ……………….. 10:46-52

7. Kuingia kwa shangwe Yerusalem …………. 11:1-11

8. Kulaaniwa kwa mtini …………………… 11:12-14

9. Kusafisha hekalu ………………………. 11:15-19

10. Kunyauka kwa mtini ………………… 11:20-26

11. Mamlaka ya Kristo ……………………. 11:27-33

12. Wakulima waovu ………………………. 12:1-12

13. Kodi kwa Kaisari ……………………… 12:13-17

14. Swali juu ya ufufuo ……………………. 12:18-27

15. Amri iliyo kuu …………………………. 12:28-34

16. Ukuu wa Yesu ………………………….. 12:35-37

17. Hukumu ya wazi juu ya waandishi ……………… 12:38-40

18. Visenti vya mjane ……………………….. 12:41-44

19. Maangamizi ya hekalu yatabiriwa ……… 13:1-37

   a. Wakati unabii ulipotolewa ………………. 13:1-4
   b. Makristo wa uongo, vita, tetemeko, na njaa ………. 13:5-8
   c. Mateso ya wanafunzi ………………….. 13:9-13
   d. Ishara ya mwisho na wakati wa kukimbia ….. 13:14-20
   e. Ishara zingine juu ya makristo wa uongo …… 13:21-23
   f. Kuja kwa Mwana wa Adam ……………….. 13:24-27
   g. Mfano wa mtini ……………………………… 13:28-31
   h. Kutokujulikana kwa siku …………………… 13:32-37

D. Kifo, mazishi, na ufufuo wa Mtumishi ……………………….. 14:1-16:20

1. Baraza na wakuu wa makuhani na waandishi …………… 14:1,2

2. Kutiwa mafuta Bethania ……………………. 14:3-9

3. Maafikiano na Yuda ……………………. 14:10,11

4. Maadalizi kwa ajili ya Pasaka …………… 14:12-16

5. Kutabiriwa kwa usaliti …………………. 14:17-21

6. Kuanzishwa kwa chakula cha Bwana ……. 14:22-26

7. Kuachwa na kukanwa kunatabiriwa ……… 14:27-31

8. Mateso katika Gethsamane ………………. 14:32-42

9. Kukamatwa kwa Yesu ……………… 14:43-52

10. Mashitaka mbele ya baraza (Sanhedrin)……………14:53-65

11. Kukana kwake Petro ………………………….. 14:66-72

12. Kushitakiwa kwa Yesu mbele ya Pilato …………… 15:1-5

13. Baraba apendekezwa na Yesu kukataliwa ..………. 15:6-15

14. Kudhihakiwa kwa Yesu na kuchukuliwa na maaskari … 15:16-21

15. Kusulibiwa ……………………………… 15:22-28

16. Kutukanwa na watu ……………………….. 15:29-32

17. Giza na hatima yake ………………………. 15:33-41

18. Mazishi ya Yesu …………………………. 15:42-47

19. Wanawake kutembelea kaburi ……………. 16:1-8

20. Yesu amtokea Mariamu Magdalena ……… 16:9-11

21. Yesu anawatokea watu wawili kijijini ……… 16:12,13

22. Agizo Kuu …………………………………… 16:14-18

23. Kupaa kwake Yesu …………………………. 16:19

24. Kwenda kwa mitume ………………………… 16:20

## INJILI YA MARKO
## MTUMISHI MWENYE MATESO

I. Matayarisho ya Mtumishi ………………………………………… 1:1-13

A. Huduma ya Yohana Mbatizaji ………………………………… 1:1-8
Linganisha Mt.3:1-12; Lk.3:4-18; Yh.1:6-8, 15-28.

Marko anampiga picha Yesu kama mchapa kazi, mwenye nguvu, mwepesi kwenda, kupigana, mfalme mwenye kushinda.

Walipowasili wafalme kwa kawaida walitanguliwa na wajumbe.

Kazi yake ilikuwa kutayaarisha njia.

Alikuwa aandaye kuja kwake.

anamwoonyesha Yohana kama mjumbe huyo.

1) Angalia jina lenye kuinuliwa lililotumika hapa:

Yesu – "Hakika ataokoa," Jina la mtu.

Kristo – aliyepakwa mafuta na Mungu ili kuwa Nabii, Kuhani na Mfalme.

Mwana wa Mungu – Mungu (Deity)!

Marko hajitaji yeye mwenyewe kuwa ndiye mwandishi.

2) *Kama ilivyoandikwa katika manabii* (KJV) [nabiii Isaya].

Marko kwanza ananukuu Mal 3:1 kuelezea kwa ukamilifu nukuu kutoka kwa Isaya.

3) *Sauti.* Hii ni nukuu kutoka Isa 40:3. Kunukuu zaidi ya nukuu mbili, na kumlenga mtu mmoja, lilikuwa jambo la kawaida.

Yohana mwenyewe alidai kuwa ni "sauti" – Yoh.1:23.

4) *Yohana alitokea akibatiza*. Ubatizo lilikuwa si jambo geni. Lilitakiwa kwa waongofu wote katika Uyahudi. Kilichokuwa kigeni ni kwamba Wayahudi, "watu wa Mungu wateule," walitakiwa kubatizwa.

*Toba liletalo ondoleo la dhambi*. εισ, inalingana na Mdo.2:38 na Mt. 26:28.

5) *Wakiziungama dhambi zao*. Angalia ubatizo (mst. 4,5), toba (mst.4) na kuungama (mst.5). Mambo haya yangetokea tu baada ya kusikia na kuamini – linga. /rum.10:14,17.

Yohana kwa hakika anatayarisha njia kwa ajili ya Kristo na kanisa, mwili wa Kristo.

6) *Na Yohana alikuwa amevalia ... akala*. Alikuwa ni mfano hai aliyejizuia katika ubinafsi wote na anasa binafsi.

Hivyo basi, alikuwa pia kinyume na mambo yasiyo na maana, kujali na amani ya uongo ambayo wengi walikuwa wakiikimbilia hata katika maafa yao.

7,8) Yohana anatoa ulinganifu aina mbili kati yake na Yesu:

Yesu ana nguvu nyingi sana (mst. 7)

Yesu ana kazi kubwa zaidi (mst. 8).

Yohana anaonyesha unyenyekevu:

Mwanafunzi anaweza kufanya takribani kila huduma.

Mtumwa (au mtumishi mnyenyekevu sana) anapenda kutumika katika kila huduma.

Yohana anajiona yeye mwenyewe kuwa hastahili kutoa huduma.

**B. UBATIZO WA YESU …………………………………… 1:9-11**

Linganisha na Mt.3:13-17; Lk.3:21,22; Yoh.1:32-34.

9) *Akabatizwa* ili kutimiza haki yote (mapenzi ya Mungu) – Mt. 3:13-17.

10,11) Nafsi zote tatu za Uungu zimekuwepo katika tukio hili kuu! Mungu daima hupendezwa na mtu yeyote kwa hiari anayemti yeye.

*Mwanangu mpendwa*. **ο υιοσ μον ο αγαπητοσ**, "Mwana wangu, mpendwa!"

C. MAJARIBU YA YESU …………………………………… 1:12,13

12) Mara. Bonde la majaribu, dhambi, na kuvunjika moyo daima ni karibu sana na kilele.

*Akamtoa aende*. **εκβαλλει,** maneno yenye kushurutisha, "alimtupa nje," – "alimtoa aende mbele."

13) *Siku arobaini* – isieleweke kama ni sawa na siku arobaini za kufunga ambazo zilitangulia kabla ya tukio hii Mt.4:2.

*Akijaribiwa na shetani*. Yesu alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi" (Ebr.4:15). Linga. 1 Yoh.2:16.

Tamaa ya mwili – amuru mawe haya yawe mikate (Mt.4:3).

Tamaa ya macho – kuonyeshwa falme zote (Mt.4:8).

Kiburi cha uzima – jitupe chini … malaika (Mt.4:6).

Kwa kujitoa kwake kwa hiari ili kubatizwa na kwa hiari kutii alipojaribiwa na Shetani, Yesu, kama Adam wa mwisho n(1 Kor.15:45), alishinda mtihani ambao adam wa kwanza alishindwa.

Yesu sasa yuko tayari kuaza huduma yake ya:

Kufundisha,

Kuhubiri,

Kuponya,

Kukemea pepo wachafu,

Kuteseka, na

Kufa kwa ajili ya kondoo.

## II. HUDUMA YA MTUMISHI GALILAYA ……………………… 1:14-9:50

### A. MWANZO WAKE ………………………………………. 1:14,15

Linganisha: Mt. 3:2; 4:12; 11:2, 14:3-5; Mk.6:17-20; Lk.3:19,20; 4:14,15; Yoh.3:24; 4:1-3, 43, 44.

14,15) *Wakati umetimia*. Kutimia kwa wakati – linganisha Gal.4:4; Efe.1:10.

*Ufalme wa Mungu* = Ufalme wa mbinguni. Linga. Mt.4:12.

Hili linaweza kueleweka kwa namna nne katika Maandiko:

Ufalme wake Mungu – Mt. 6:10.

Wokovu – Mk.10:25,26.

Kanisa – Mt.16:18,19.

Mbinguni – Mt.25:34.

*Tubuni na kuiamini injili*. Mabadiliko katika mfumo wa akili na "kuamini" inaonyesha mwelekeo – upande wa injili.

### B. KUITWA KWA WAVUVI WANNE …………………. 1:16-20

Linganisha: Mt. 4:18-22; Lk.5:10.

16-20) Iwapo pana maendeleo yoyote makubwa lazima yatokane na wale "walio sakafuni chini," wanaoitwa kwa mara ya kwanza na kushika nafasi za uongozi. Viongozi na watu wote maarufu wana wafuasi wao wa karibu.

### C. KUPONYWA KWA MWENYE PEPO MCHAFU …… 1:21-28

Linganisha: Lk. 4:31-37.

22) *Alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi*. Wala si rabi au mwalimu aliyewahi kufundisha katika amri yake. Walinukuu kutoka kwa wengine na mapokeo yao. Lakini Yesu anazungumza kwa amri ya Uungu, chemichemi za maji ya uzima – Yer.2:13.

23) *Mtu mwenye pepo wachafu*. Je pepo wachafud huwapagawa watu siku hizi? HAPANA! Mambo haya yalikuwa kwa kitambo na yalikoma wakati uwezo wa kuyakemea ulipobatilkika – Yoh.20:30,31; 1 Kor.13:8-13; cf. Zek.13:1-3.

24) *Ondoka tuache peke yetu! Tuna nini nawe*? Pepo mmoja anazungumza kwa niaba ya wengine, akitambua kwamba kitakachompata yeye ni fungu la pepo wote. Linga. Yak.2:19.

25) *Fumba kinywa*. Yesu hakuwa na haja ya mwovu huyo kumshuhudia. Iwapo angeruhusu jambo hili kendelea lingeleta mashaka katika madai na ujumbe wa Yesu.

26) *Akamtia kifafa*. KJ V ya kale – akamlarua "torn him." Na NKJV iko sahihi. Hakudhuriwa kimwili. Neno hili limetafsiriwa kifafa (epileptic) katika Mt.17:15.

28) *Habari zake zikaenea*. Matendo makubwa huleta kujulikana mno.

D. **KUPONYWA KWA MAMA MKWE WA SIMONI NA WENGINE WENGI ……………………………… 1:29-34**

Linganisha: Lk. 8:14-17; Lk.4:38-41.

31) Luka ameongeza “akaikemea ile homa.” Yesu alitumia nguvu zake kuishinda homa kabisa, dhoruba, na asili zote. Neno lilo hilo limetumika katika Lk.8:24.

Mathayo anabainisha kwamba hayo yalitendeka ili kutimiza Isaya 53:4, “Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu.”

**E. WATU WOTE WANAKUTAFUTA ………………………1:35-39**
Linganisha: Lk.4:42-44, pia Mt.4:23-25 pamoja na Mk.1:39.

35) Yesu aliona umuhimu na hitaji la sala. Aliomba mara nyingi, kama vile:

| | |
|---|---|
| Katika ubatizo wake | Lk.3:21 |
| Kuchagua kumi na wawili | Lk.6:12 |
| Kulisha elfu tano | 6:41, 46 |
| Mlimani alipogeuka sura | Lk.9:28 |
| Muundo wa sala | Lk.11:1 |
| Katika kumfufua Lazaro | Yoh.11:41,42 |
| Kwa ajili ya Petro, kabla ya kumkana | Lk.22:32 |
| Katika Gethsamane | Mk.14:32-39 |
| Msalabani | Mk.15:34 |
| Baada ya ufufuo wake | Lk.24:30 |

Etc., etc.

Sala haiwezi kutekeleza kazi zetu; kinachofanywa na sala ni kututia nguvu tupate kufanya kazi ambayo ni sharti tuitimize.

38) Nipate kuhubiri huko nako. Yesu hasemi lolote juu ya kutenda miujiza katika maeneo haya, bali mkazo wake mkubwa ni katika kuhubiri “ufalme wa Mungu” (Lk.4:43).

### F. MWENYE UKOMA APONYWA …………………………1:40-45

Linga. Mt. 8:2-4; Lk.5:12-16.

41) Upendo na uweza wa Mungu, ndani ya Yesu, ulidhihirika mara kwa hitaji na ombi la mwenye ukoma.

Yesu hakumfukuza mtu huyo alivunja sheria kwa kumjia (kama mkoma).

Yesu alimgusa mtu huyo aliye najisi.

Baada ya kuponywa, Yesu akamtuma kwa makuhani ili kutimiza sheria.

43,44) *Usimwambie mtu neno lolote*. Yesu alitaka ajulikana kama mleta ujumbe wa Mungu na wala si mtenda miujiza.

Hilo lingesababisha usumbufu kuja mapema kabla ya wakati wake kutimia.

Ukajionyeshe kwa kuhani. Mambo mawili makuhani wangejua kama matokeo ya jambo hili:

Ushuhuda isiopingika kwa uwezo na upendo wa Yesu.

Yesu anashutumu mapokeo ambayo huiharifu Sheria, kwa sababu anaitii Sheria na kumwamuru mwenye ukoma kuitia pia.

### G. KUPONYWA KWA MWENYE KUPOZA ……………. 2:1-12

Linganisha: Mt.9:2-8; Lk.5:17-26.

Sura 1 ni moja ya sura ya utukufu wake Yesu, lakini sura 2 inaanza na mgongano. Mgongano usingeepukika.

| Yesu alitia mkazo: | Wayahudi walitilia mkazo: |
|---|---|
| Upendo | Mambo ya sheria (legalism) |
| Sheria takatifu za Mungu | Sheria – ikishinda uhalalisho |
| Uhuru | Utumwa |

Utu wa ndani Matendo ya nje

Wangelichukia kutokupewa heshima na nafasi zao hadharani.

5) Mwanangu, umesamehewa dhambi zako. Wayahudi wakati wa Yesu walidhania kuwa ugonjwa ililetwa na dhambi. Yesu haungi mkono maoni yao, bali anaonyesha kuwa alikuwa na uwezo wa kusamehe dhambi.

Wayahudi walisadiki mtu asingeliweza kuponywa hata dhambi zake zisamehewe.

Mtu aliponywa. Kwa hiyo, alikuwa amesamehewa.

Hivyo basi, madai ya Yesu ya kuwesa kusamehe dhambi sharti yawe ya kweli.

Yesu ameingia katika mapambano na kwa kutimiza malengo yote, “ametia muhuri kibali cha kifo chake mwenyewe.”

**H. KUITWA KWA LAWI ………………………… 2:13-17**

Linganisha: Mt.9:9-13; Lk.5:27-32.

14) *Ameketi forodhani* – Kibanda chake cha kukatia ushuru, mahali ambayo kodi zilikusanywa kwa mfanya biashara yeyote aliyepita hapo katika njia kuu ya kimataifa kati ya Shamu na Misri.

16) *Mbona anakula na pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi*? Kwa Mafarisatyo mwenye dhambi ni yeyote aliyekataa kutii tafsiri yao ya Sheria.

Kwa maana hiyo, Yesu alikuwa “mwenye dhambi” kwa mtazamo wao.

Lakini, mmoja wa wenye “dhambi” hawa sharti haswa ahesabiwe haki mbele ya macho ya Mungu.

Yesu anatuonyesha kuwa wakati fulani “ushirika” unahitajika ili kuwaleta kwa Mungu.

17) Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi, ili watubu. Watu hawa walijidhania kuwa wenye haki, lakini Yesu anawaonyesha ukweli mkubwa.

Kufikiri kwamba hatuhitaji msaada ni kujenga ukuta kati yetu na Yesu.

Kufikiri kwamba tunahitaji msaada ni kuwa na “kibali” (passport) kwa kuwepo kwake.

### I. SWALI JUU YA KUFUNGA ……………… 2:18-22

Linganisha: Mt.9:14-17; Lk.5:33-39.

19,20) *Muda wote walipo na bwana-arusi hawawezi kufunga … ndipo watafunga siku ile*. Katika Mt.9:15 panasema, "… watakapoondolewa bwana-arusi," anarejea Isa 53:8.

Marko anarejea mara nyingi katika Isaya:

| Marko | Isaya: |
|---|---|
| 2:20 | 53:8 |
| 4:12 | 6:9,10 |
| 7:6,7 | 29:13 |
| 9:12 | 53:3 |
| 11:17 | 56:7 |
| 12:1 | 5:1,2 |
| 13:8 | 19:2 |
| 13:24,25 | 13:10; 34:4 |
| 15:4,5 | 53:7 |

Ulikuwepo utawala wa Kirabi (rabbinic ruling): "Waliohudhuria wote waalikwa na bwana-arusi wako huru na makatazo yote ambayo yangelipunguza furaha yao." Waalikwa wote katika arusi waliruhusiwa kutokufunga.

21,22) Yesu anachosema ni kwamba akili za dini ya kizamani, iliyotangulia, kali ya Kifarisayo haiwezi kupokea ukweli mpya anaowajia. Dini mpya ya Kristo itawajia wanadamu pale tu akili na mioyo yao itakapokuwa wazi kupokea injili.

### J. BWANA WA SABATO ………………………………. 2:23-28

Linganisha: Mt.12:1-12; Lk.6:1-5.

Yesu anatilia mkazo kwamba hao waliopo walio hai mbele zake walipaswa kusherekea, na wala si kufunga; kufurahia, na wala si kuomboleza.

Walikuwa wakifanya si kuvunja Sheria ya Musa. Kwa kadiri msafiri ambapo hakupeleka mundu katika shamba la nafaka la mtu, aliruhusiwa kutwaa baadhi na kula – linga. Kumb. 23:25.

Mwanadamu aliumbwa kabla ya sheria ya Sabato. Mtu hakuumbwa kuteswa na kuwa mtumwa na sheria za Sabato na maagizo yaliundwa na viongozi wa dini.

Mwanadamu hakupaswa awe mtumwa wa Sabato; Sabato ilikuwepo ili kuyafanya maisha yake yawe bora zaidi.

Yesu ni mkuu kuliko:

Hekalu - Mt.12:6

Baadhi wamejaribu kuonyesha kuwa ni kahaba katika Lk.7:37ff, lakini hakuna uhakika wa jambo hilo!

**R. MAZIKO YA YESU …………………………………….. 15:42-47**
Linganisha: Mt.27:57-66; Lk.23:50-56; Yoh.19:38-42

Wayahudi walikuwa tayari wamechukua hatua ya kuondoa miili kabla ya Sabato. Kama mpango wa Wayahudi ungekuwa umetekelezwa, mwili wa Bwana ungekuwa umepelekwa katika makaburi ya watu wa kawaida sehemu ya wakosaji waliogongomelewa.

Mbali na ukweli kwamba Yesu alikuwa amesulibiwa kwa sababu ya uhaini na kwamba Yusufu alikuwa hana uhusiano naye, kwa ujasiri alimwomba Pilato ampatie mwili wa Yesu ili akamzike.

Kwa uhodari Yusufu alikuwa amekubali matokeo yoyote yale ambayo yangempata!

Kusema ukweli, wanadamu wanatakiwa waonyeshe msimamo ama kwa kuwa pamoja na Kaisari au pamoja na Kristo – hakuna kuwa vungu-vungu (middle ground)!

Linga. Kumb.21:23.

Kufa kutokana na kusulibishwa kwa kawaida kulichukua siku mbili au tatu baada ya kupigiliwa msalabani. Katika matukio mengine aliyesulibiwa haswa alikufa kwa njaa mbali na vidonda vyake.

Bila masharti Pilato akampatia Yusufu mwili wa Yesu kwa namna hii, na ukazikwa kama ilivyokuwa, hapakuwa na mawazo yoyote kwamba angefufuka.

Linganisha Isaya 53:9.

*Wakapatazama*. Yaani kuzingatia kwa makini na kwa uangalifu.

**S. KUTEMBELEA KABURINI KWA WANAWAKE ……………… 16:1-8**
Linganisha: Mt.28:1-8; Lk.24:1-8; Yoh.20:1-10

Hii ni kazi ya upendo kwa wanawake hawa, bali pia ni kazi ya kutokuamini. Kwa hali yoyote ile, je, Yesu hakuwaahidi kwamba angefufuka toka kwa wafu siku ya tatu?

Ukweli kwamba hawakutarajia yeye kufufuka hilo hutoa ushuhuda wao zaidi.

Wanawake hawa wanaonekana kutokujua mpango wa Wayahudi na Pilato. (Wayahudi walimwendea Pilato, walilifunika kaburi na jiwe, na kuweka walinzi juu ya kaburi.) Wanachojali hapa ni jinsi gani wataweza kuliondoa jiwe kaburini.

Jiwe halikuviringishwa ili kumtoa Yesu nje. Hakuhitaji kutolewa nje. Jiwe halikuwa kikwazo kwa Yesu, bali lingekuwa kikwazo kwa wanawake na mitume.

*Wakastaajabu*. Haya yalikuwa ni maajabu, wala si kuogopa.

Malaika si maono. Alizungumza na wanawake, akiwajibu maswali ambayo wala hawakuuliza.

Aliyesulibiwa. Ainisho hili la aibu yake sasa limefanywa kuwa taji ya utukufu wake.

*Enendeni … mkawaambie*. "Ukweli kwamba wanawake ndio walikuwa wa kwanza kupokea tangazo la ufufuo ni swala la msingi kutokana na tabia za wakati huo. Sheria za Kiyahudi zilisema kwamba wanawake hawakustahili kutoa ushahidi. Historia ya Wakristo wa kwanza inathibitisha kwamba taarifa za wanawake juu ya kaburi wazi na ufufuo wa Yesu zilitazamwa kama za aibu (linga. Lk.24:11, 22-24; Mk.16:11). Kwamba habari zililetwa na wanawake kwanza hazikufaa na zikaleta matatizo katika kanisa, kwa maana ushuhuda wao ulikosa thamani ya kuwa ushahidi thabiti. Jamii hii ya kale isingevumbua maelezo haya, ambayo yanaweza tu kubainishwa katika msingi wa kuwa ni ya kweli." W. L. Lane.

Mkamwambie …. Petro. Petro alikuwa amemkana Bwana wake. Hili lingempatia ujasiri wa pekee na ufahamu kwamba alikuwa bado na thamani kwa Bwana na kazi yake.

Galilaya. Hili lingeliwakumbusha mitume mambo ambayo Bwana aliwaeleza mahali pa kumkuta. Kwenda Galilaya pia kungewaondolewa mawazo ya kuanzisha ufalme Yerusalem.

Waliongopa kubakia mbele za malaika baada ya kuwaachia agizo ya kuondoka na kupeleka ujumbe kwa mitume na Petro.

Watu wanapokuwa wamekabiliwa na Mungu moja kwa moja katika mambo yao duniani hapa, hajui la kufanya. Ufunuo wa Mungu na kuingiliwa kati ni nje na uwezo wa mwanadamu na hatuna ujuzi wowote katika maisha yetu ambao utatusaidia kuelewa na kujibu barabara. Mara moja mwanadamu anazidiwa na hofu.

## T. YESU ANAMTOKEA MARIAM MAGDALENA ………………….. 16:9-11

Linganisha: Mt.28:9,10; Yoh.20:11-18

*Hawakusadiki*. Wazo hapa si kwamba hawakuamini bali ni kwamba walikataa kuamini. Hili pia linadhihirisha jinsi walivyohofu hata kutokuwa na matumaini. Hata ingawa walielezwa kwamba angefufuka hawakuamini ingekutokea hivyo.

**U. YESU ANAWATOKEA WAWILI ………………………. 16:12,13**
Linganisha: Lk.24:13-35

*Ana sura nyingine*. Maneno haya haswa, "Kwa namna nyingine nje jinsi sura ilivyoonekana."

**V. AGIZO KUU ……………………………… 16:14-18**
Linganisha: Mt.28:18-20; Lk.24:36-49; Yoh.20:19-23

Baada ya Yesu kusulibiwa wanafunzi wake walitawanyika, matarajio yao yakatoweka kwa mambo yaliyotokea. Kikundi kizima cha Masihi kingefikia kilele kama Yesu asingelifufuka!

Hili linaitwa "agizo" kwa sababu linawapa mitume agizo ambalo hawajawahi kuwa nalo hapo nyuma – mamlaka ya kuhubiri injili na kuueleza ulimwengu mpango wa wokovu.

*Ataokoka*. Neno hili pia linamaanisha "salimisha." Linamaansha kusalimisha, maana yake kilichokuwa hatarini au katika dhiki, na hatari hiyo au dhiki imeondolewa.

*Kubatizwa*. Kama kuna mtu anapinga ubatizo kuwa unahusishwa katika wokovu na akumbuke kwamba ni Yesu mwenyewe ambaye anayeunganisha pamoja maneno hayo mawili. Tunaasi katika wazo hili, makosa yote ni yetu mwenyewe!

Kama liwali wa jimbo angetoa msamaha kwa wafungwa iwapo wangetia sahihi fomu kwamba wangelikuwa raia wema na wangebatizwa ili kuthibitisha mkataba, pasingelikuwepo na mfungwa ambaye angeamini kwamba kinachotakiwa tu ni kutia sahihi karatasi, lakini hautakiwi kuzamishwa.

"Hukumu huwakalia wao wasioamini (Yoh.3:18), Lakini mitume hapa wameelezwa kwamba itakuwa juu ya wanaosikia injili na hawaamini. Iko juu yao sasa, na sharti, hakika, iwe juu yao milele isipokuwa, kama baadaye katika uhai, wataamini. Kwa jinsi hii hali yao ya hukumu ambayo ipo sasa itafika hata milele, isipokuwa kikiondolewa kinachosababisha, namna hiyo hiyo ndivyo ilivyo hali ya wokovu unavyofurahiwa na wenye kuamini na

kubatizwa utakwenda hata milele, isipokuwa baadaye ukipotezwa kwa ukengeufu." C.E.W. Dorris.

Pia linganisha Yoh.3:36.

Pengine swali linaweza kuulizwa, "Mungu anawezaje kuwa wa haki kwa kuwahukumu watu kutokana na kutokutii injili?" Ninajibu swali –

1. Mungu ana haki ya kuchangua njia zake za rehema.

2. Mwanadamu hana madai ili apate mbingu.

3. Mwenye dhambi anakataa njia ya jinsi ya wokovu, kwa kujua kwake, kwa hiari, na akidumu kukana.

4. Hajali na kudharau kabisa injili.

5. Kutokuamini kwake injili kumetokana na kupenda kwake dhambi.

6. Anadhihirisha kwa hilo kwamba hana upendo kwa Mungu na Sheria zake, na kwa ajili ya milele.

7. Amedharau makusudi ya Mungu na haswa mwanadamu aliye mfano wake, na

8. Lazima awe na huzuni. Kiumbe asiye na matumaini katika Mungu; ambaye hasadiki kwamba yeye ni kweli na mwenye kustahili heshima yake, ambaye hatafuti kamwe rehema zake, lazima awe na huzuni nyingi. Anamkataa Mungu, na ni lazima aingie katika umilele akiwa hana Baba au bila ya Mungu. Hana chimbuko la faraja katika maisha yake, na lazima afe milele. Hakuna kiumbe kingine kilicho cha milele isipokuwa Mungu ambaye anaweza kumfanya mwanadamu kwa na furaha, na bila ya rehema zake, mwenye dhambi sharti awe na huzuni nyingi." A. Barnes.

Asiyeamini amehukumiwa ama akibatizwa au asipobatizwa!

Neno "kuokoka" linapotumika likimaanisha hali ya kuokoka katika maisha haya (Mdo.2:47; 1 Kor.1:18; 15:2; Efe.2:5; Tit.3:5) linamaanisha kwamba tumekuwa salama kutokana na dhambi zetu za kale. Hali hii imewezeshwa na msamaha wa Mungu na hauwezekani kupokelewa kwa namna nyingine yoyote ile.

Ishara hizi. Ahadi hii haielezi ni muda gani haswa ishara hizi zingedumu, wala haielezi ni kwa kila mtu atakayeamini. Inamaanisha tu kwamba zitawafuata hao waaminio kwa ujumla.

Ishara hizi hazikuambatana nao walioamini siku za mitume. Hazikuabatana na kila aliyeamini bali zikuwa karibu katika kila mwili (kanisa) wa waumini kila mahali walipokuwa. Hili lilikuwa utimilifu haswa wa ahadi zake, na yeyote anayedai kuwa ahadi inajumuisha wengine zaidi anasisitiza nje na ahadi ilivyokusudiwa na umuhimu wa kutekeleza maana yake.

Kusudi la ishara hizi ilikuwa kulithibitisha agizo ambalo lilitolewa kwa kanisa na hazikukudiwa kuwa uthibitisho wa imani ya mtu yeyote binafsi.

Katika jina langu – kwa mamlaka yake na kutumia nguvu ambazo angezitumia kama angekuwepo kimwili wakati huo.

Linganisha: Mdo.28:3-6

**W. KUPAA KWAKE YESU ………………………….. 16:19**

Linganisha: Lk.24:50-53

Mkono wa kuume wa Mungu. Inamaanisha kuwa Yesu ameinuliwa kwa kupewa heshima na uweza, na kukaa pamoja na Baba mbinguni.

Hii ni heshima ya juu kupita zote, au kuliko popote, ambayo inaweza kupewa Mwokozi wetu.

**X. MITUME WAKAONDOKA ……………………….. 16:20**

Wakahubiri kote kote – wakifanya kazi kwa kushirikiana pamoja, kuungana pamoja.

Bwana akitenda kazi pamoja – kwa njia ya miujiza (ishara), kwa kuondoa vikwazo, kwa kuwasaidia, na kuifanikisha injili na kuifanya iwe na matunda katika kuwaokoa wanadamu.

*************MWISHO **************